## Majibu ya KCPE, 2010

# RIWAYA MPYA YASISIMUA

**Na HUGHOLIN KIMARO**

RIWAYA mpya ya Heri Subira ya Omar Babu iliyochapishwa na matbaa ya Oxford inatarajiwa kuwa tishio kubwa kwa 'Siku Njema' ya Ken Walibora.

Heri Subira ina uzuri wa kipekee ambao utaipa nafasi nzuri ya kushindana na 'Siku Njema' ambayo inasifika kwa kiwango chake cha juu cha usanifu wa lugha, matumizi ya mbinu tele za usanii na mtiririko mwanana wa vitushi katika riwaya nzima.

Bila shaka ni kutokana na ubora huo wa riwaya hiyo uliifanya ipendekezwe na kuwa miongoni mwa vitabu vya fasihi katika Mtihani wa Kidato cha Nne (KCSE) kwa miaka kadha.


Kuingia sokoni majuzi kwa 'Heri Subira' kwa kishindo kulinirejesha nyuma nikakumbuka nilivyovutiwa na 'Siku Njema' nilipoisoma kwa mara ya kwanza.

Kimuhtasari, mwandishi anatusimulia mengi kuhusu maisha ya Sabra, bintiye Mzee Fauz na Mama Khadijah walioishi mtaa wa Tamakani.

Kama ilivyokuwa desturi, mabinti wa enzi hizo walitawishwa na wazee wao. Hawakuwa na uhuru wa kutoka na kwenda kutangamana na vijana wenzao walipotaka. Mzee Fauz anashtuka sana siku ya kwanza anapogundua kuwa Sabra anashirikiana na na wanafunzi wenzake wa kiume wakati wa kudurusu kwa mtihani na kutoka shuleni wakiwa wamechelewa.

Mzee Fauz haamini kabisa kuwa bintiye anaweza kujiamulia jambo lolote la maana kuhusu ndoa. Hivyo, kama ilivyokuwa desturi enzi hizo anamtafutia bintiye mume na kumwoza.

Hii inafanyika ingawa kulingana na matokeo yake angeweza kuendelea na masomo ya chuo kikuu kwa kujigharimia. Alijua vile hali ilivyokuwa kwani hata masomo yake ya sekondari aliona jinsi babake alivyojikokota



Riwaya ya Heri Subira Picha/ HUgholin Kimaro

katika katika kumsomesha. Si kwamba hakuwa na uwezo wa kumsomesha, la, ni kwamba tu hapendi kuelimisha watoto wa kike.

Lisemwalo lipo na kama halipo laja. Siku moja Sabra anawaona watu wamewasili nyumbani na anaarifiwa kuwa ni wageni wake. Kumbe ilikuwa ni posa yake iliyoletwa.

Waliosema ushikwapo shikamana hawakukosea. Wazazi wake Sabra waliposhikilia msimamo wao kwamba sharti aolewe aliafikiana nao na kuolewa kwa mume tajiri aliyechaguliwa - Khalid.

Kulingana na mwandishi

Uk 26: Khalid alikuwa jamali, mrefu na mwenye kifua kipana. Umbo lake lilikuwa smaku tosha kwa mabanati. Ukiongea na huo utajiri ambao Sabra alikuwa hajauonja bado, binti ambaye angempata angekuwa chambilecho wajuzi, 'ameukata.'

Ingawa Khalid alikuwa mzuri kiasi hicho roho ya Sabra haikumpenda. Sababu yenyewe Sabra hakuijua.

Harusi ya kifahari iliandaliwa na Sabra akaolewa.

Ajabu ni kwamba hata siku ya kwanza ya ndoa Khalid hakulala kwake nyumbani. Anamwacha Sabra katika hali ya upweke anaenda kusikojulikana na kurudi asubuhi na tabia hii anaiendeleza.

Sabra anapolalamika hapati jibu la kuridhisha na mwisho anapigwa ili anyamaze. Maji yanapozidi unga analalamikia wazazi wa pande zote mbili bila mafanikio.

Hali inapoharibika kabisa anatoroka na kwenda kujificha kwa Biti Baraka, bibi kizee aliyekuwa mtumishi wao wa nyumbani zamani. Kwa sasa bibi huyo aliishi mtaa wa Mayoweni.

Kisadfa, Sabra anakutana na Heri mwanamume mwenye utu wa kweli ingawa hakujulikana asili wala fasili, urafiki baina yao ukatunga na mwisho wakaoana bila idhini ya Mzee Fauz.

Bila kujua, Heri anamwokoa Mzee Fauz kwa kumtolea figo lake moja anapokuwa mgonjwa na hatua hii inaleta urafiki na udugu mpya; familia ya Fauz inawasamehe kwa yote yaliyopita. Mzee Fauz alifurahia sana kumwona Fauz mdogo (mwanawe Sabra na Heri).

Kiwango cha ubunifu, mbinu za usanii na lugha zilizotumika ni za hali ya juu na zimeifanya kazi yenyewe kuwa kivutio kikuu. Msomaji atakaye kuyaona matumizi mwafaka ya taharuki, majazi, tashbihi, uzungumzi nafsia, kejeli, kinaya, semi na kadhalika atayapata katika riwaya hii.

Maudhui na dhamira anayotufikishia mwandishi katika riwaya ni mwongozo muhimu katika maisha yetu.

Ni riwaya safi sana kwa wanafunzi wa fasihi katika kiwango cha KCSE na pia vyuoni.

Akieleza kuhusu riwaya ya Heri Subira, Bw. Hezekiel Gikambi, ambaye alifaidika kuipitia riwaya hiyo ikiwa mswada mbichi, alisema kuwa alivutiwa sana na jinsi Omar Babu alivyofanikiwa katika 'kuchora taswira ya wahusika na mandhari kwa kusuka hadithi inayotuletea uhalisia wa Uswahilini uliomichiwa lulu na pilipili za usasa'.

'Taswira ni mbinu ambayo hufanya miujiza ukiweza kuitumia kwa ufasaha katika kazi yoyote ya kifasihi', akaongezea Bw. Gikambi ambaye pia ni mwandishi na mhariri wa vitabu na magazeti. Heri Subira ni baadhi ya riwaya chache za kisasa zilizo na ukurasa katika Facebook.

Maoni kwa:*hkimaro@ke.nationmedia.com*

## MAJIBU YA KCPE, 2010

**Majibu ya mtihani wa KCPE KISWAHILI JARIBIO la Saba uliochapishwa 02/11/2010**

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | D | 11. | C | 21. | B | 31. | B | 41. | B |
| 2. | B | 12. | B | 22. | B | 32. | D | 42. | D |
| 3. | C | 13. | D | 23. | D | 33. | A | 43. | A |
| 4. | A | 14. | B | 24. | B | 34. | C | 44. | B |
| 5. | A | 15. | C | 25. | D | 35. | B | 45. | C |
| 6. | C | 16. | D | 26. | D | 36. | D | 46. | C |
| 7. | D | 17. | A | 27. | C | 37. | A | 47. | D |
| 8. | B | 18. | D | 28. | B | 38. | A | 48. | A |
| 9. | A | 19. | C | 29. | A | 39. | C | 49. | D |
| 10. | C | 20. | A | 30. | A | 40. | D | 50. | B |

**KWA WANAFUNZI, WALIMU NA WASOMAJI WETU WOTE**

**Kutokana na idadi ya maelfu na maelfu ya insha tunazopokea kwa 'Shindano la Insha la Taifa Leo' kutoka kote nchini Kenya na maombi waliyotuma walimu wa shule mbali mbali, tumeonelea kuwa badala ya kuichapisha insha bora zaidi gazetini, tuongezee orodha ya wanafunzi walioandika insha bora kutoka 20 bora hadi 50 bora nchini. Hii itawapa nafasi wanafunzi na walimu kuona bidii yao iliwafikisha wapi. Shindano hili linaendelea. Mshindi wa kwanza wa insha bora zaidi ndiye hutuzwa zawadi ya Sh1000, mwalimu wake Sh1000 na shule Sh3000.Wanafunzi 50 bora nchini wataorodheshwa kila baada ya wiki mbili. Masharti yetu yatazingatiwa kikamilifu.**

TAIFA LEO | TOLEO LA ELIMU




JIIMARISHE KIELIMU SASA!

MITIHANI HII ITATOKEA JUMATATU NA JUMANNE NA MAJIBU YAO KUTOKEA ALHAMISI NA IJUMAA

TAIFA LEO

USIKOSE NAKALA YAKO KUANZIA 5, APRILI - 9, NOVEMBA 2010